JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'

**Simu Na**:-

**(i) Mkuu wa shule**
0786 – 717019
0625 – 417019

**(ii) Makamu mkuu wa shule**
0786 – 190 252
0688 – 980641

**(iii) Mwl Taaluma**
0683 – 366970

NANGWA SEKONDARI,
S.L.P 34,
**KATESH – HANANG'.**

**Tarehe 26/04/2024**

**Email addresses:-**

**(a) Ya shule -**
**nangwa@hanangdc.go.tz**

**(b) Ya mkuu wa shule-**
**manyaadelina@gmail.com**

Unapojibu tafadhali taja:-
Kumb. Na. NSS/ADM/J.INSTR. FV/VOL.I/2023

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI:-
…………………………………………..
S.L.P …………………………………….
…………………………………………..

YAH**:** MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA TANO SEKONDARI YA WASICHANA NANGWA HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG' MJI WA KATESH MKOA WA MANYARA MWAKA 2024/2025.

**1.** Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano (kdt V) katika shule hii (Nangwa sekondari) mwaka **2024** tahasusi ya HGE/HGL/HGK/HKL/CBG/PCB.

Shule ya sekondari ya wasichana Nangwa ipo umbali wa **kilometa kumi tu** (10km) kutoka makao makuu ya wilaya Mashariki mwa mji wa **Katesh,** usafiri wa mabasi kutoka mjini Katesh unapatikana katika kituo cha mabasi cha Katesh nauli ni shilingi elfu moja tu (Tshs 1,000/=).

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **01.07.2024** mwisho wa kuripoti ni tarehe **14.07.2024**

# HONGERA SANA!!!!

# Mahali shule ilipo.

Shule ya sekondari ya wasichana Nangwa ipo Mkoa wa **Manyara** wilaya ya **Hanang'** mji mdogo wa **Katesh,** Tarafa ya **Katesh**, kata ya **Nangwa**, kijiji cha **Mlimani,** kitongoji cha **Nangwa juu.**
Usafiri wa mabasi kutoka mikoa mbalimbali unapatikana muda wote.
Shule ipo umbali wa kilometa moja na nusu tu (1.5) kutoka barabara kuu itokayo Arusha - Singida au Singida - Arusha.

- Wale watokao kanda za kusini, nyanda za juu kusini, kati na Mashariki (Iringa, Mbeya, Rukwa, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Dodoma, Morogoro na Dar- es- salaam) njia rahisi ni ile inayopitia Dodoma – Babati hadi Katesh. Itawalazimu kushuka kituo kidogo cha mabasi kiitwacho Nangwa **kabla** ya kufika kituo kikuu cha mabasi cha **Katesh.Iwapo utapita njia ya Singida itakulazimu kushuka Nangwa baada ya kituo cha mabasi Katesh.**
- Wale watokao kanda ya Magharibi na ziwa (Mwanza, Shinyanga, Tabora, Musoma, Geita na Simiyu). Njia rahisi kwao ni ile inayopitia Singida – Katesh. Itawalazimu kushuka kituo kidogo cha mabasi kiitwacho Nangwa **baada** ya kituo kikuu cha mabasi **Katesh.**
- Wale watokao Kanda za Kaskazini Magharibi, Kaskazini na Mashariki (Tanga, Kilimanjaro na Arusha). Njia iliyo rahisi kwao ni ile inayopitia Arusha – Babati hadi Katesh. Hawa itawalazimu kushuka kituo cha mabasi kidogo kiitwacho Nangwa **kabla** ya kituo kikubwa cha mabasi kiitwacho **Katesh.**

***Nawatakia safari njema!!!!***

# KARIBUNI SANA.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare ya shule**

**(i) Sare ya darasani.**

- Sketi suruali mbili (2) rangi ya blue bahari, kitambaa kizito, mshono wa heshima, marinda ya upanga kumi na mbili (12) **(nyuma rinda sita na mbele rinda sita)**. Zipu ikiwa pembeni kushoto na mfuko kulia. Kitambaa kiwe kikubwa kinachoruhusu marinda mazuri yenye kujimwaga hadi chini ya sketi,
  urefu wa sketi ni inchi sita (06) kutoka magotini kwenda chini. "Belt" yenye inchi mbili (02) na pindo la chini liwe la wastani.

***NB: Kitambaa na picha ya mshono wa sketi vimeambatishwa pamoja na fomu hii. Angalia (Kiambatisho A).***

- Mashati meupe mawili ya tetron yenye mikono mirefu.
- Tai mbili "dark blue" fupi kiasi na pana pamoja na pini yake.
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi.
- Sweta rangi sawa na sketi mshono wa V kwenye shingo.
- Soksi ndefu nyeupe jozi mbili

**Iwapo mwanao ni mwislamu sare ya shule itakuwa ni:-**

- Suruali mbili (2) zisizobana rangi ya blue bahari.
- "Short" kanzu mbili (2) nyeupe urefu ni inchi kumi na mbili (12) kutoka gotini kwenda chini, pana isiyo na mipasuo pembeni.
- Hijabu (kijuba) mbili (2) "ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

**(ii) Mavazi ya kazi (shamba dress).**

- Sketi suruali mbili (2) nyeusi nzito mshono kama sketi za darasani.
- Waislamu suruali mbili (2) "short" kanzu nyeusi mbili (2) urefu ni kama ilivyofafanuliwa hapo juu pamoja na hijabu (kijuba) nyeusi mbili (2).
- Mabuti ya mvua meusi au ya kijani jozi moja tu.
- Mwavuli mmoja (1) kwa wote kwa ajili ya kujikinga na mvua kipindi cha masika.
- Raba nyeupe au nyeusi **(mwanafunzi huruhusiwi kuvaa ndala nje ya bweni au darasani.)**

**NB. Ndala zitatumika ndani ya bweni tu kwa matumizi ya kuoga.**

Vazi la kazi litavaliwa na "T-shirt" yenye nembo ya shule ambayo mzazi/mlezi unatakiwa kuileta na itagongwa nembo ya shule hapa shuleni.Kwa waislamu watavaa "Tshirt" ndani ya "Short" kanzu nyeusi.

**(iii) Mavazi kwa ajili ya kuzuia baridi (nje ya darasa)**

- Pull neck mbili (2) nyeupe nzito zisizo na maandishi wala madoido yoyote.
- Sweta mbili (2) rangi ya "dark blue" zisizo na maandishi mshono wa V shingoni

**NB: Mzazi/mlezi utawajibika kumshonea mwanao sare zote kama zilivyotajwa hapo juu na mwanafunzi ajapo shule awe amevaa sare za darasani kinyume cha hapo hatapokelewa.**

**(iv) Sare za michezo**

Kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki michezo.

**Michezo ni lazima na ni somo mojawapo linalotiliwa mkazo na kuthaminiwa sana hapa shuleni.**

**Hivyo mwanafunzi itamlazimu aje na vifaa/nguo vifuatavyo/zifuatazo ili kufanikisha shughuli za michezo:-**

- T-shirt rangi ya blue iliyokolea pamoja na bukta au suruali ya blue iliyokolea, sketi ya blue iliyokolea fupi usawa wa magoti ambayo itavaliwa juu ya bukta au suruali, "**sketi hiyo iwe ya *mshono wa solo"***.
- Track suit rangi ya blue bahari nzito.
- Mwanafunzi anatakiwa aje na godoro la futi $2\frac{1}{2}X3$ au Shilingi 5,000/= kwa ajili ya kukodisha godoro kwa muhula.
- Raba jozi moja (01) za michezo "njumu".
- Soksi za michezo jozi mbili (02)

### 2.2 Michango mbalimbali

#### (a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:-** Michango yote ilipwe kwenye akaunti ya shule **Na. 41001200070** katika benki ya NMB tawi lolote, Jina la akaunti ni **Akaunti ya Ada Nangwa sekondari** Mwanafunzi atatakiwa kuleta "Bank Pay In slip" **(BPS)** iliyoandikwa jina kamili la mwanafunzi yeye mwenyewe na si jina la mzazi, mlezi au aliyetuma fedha.

**Angalizo:-Hatupokei fedha taslim na fedha zikishawekwa kwenye Akaunti hizo zilizotajwa hapo juu hazirejeshwi.**

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

(i) Rim mbili (02) za karatasi kwa mwaka aina ya Rotatrim ($A_4$).
(ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (kama ilivyo katika kiambatisho D)
(iii) Mashuka 2 rangi ya blue bahari, blanketi 1, foronya 2 rangi ya blue bahari pamoja na mto wa kulalia mmoja 1, chandarua 1 nyeupe au blue 'pembe nne au duara'. Aje na taulo, nguo za kulalia "night dress" mbili (2), sanduku moja (tranka) moja tu lenye kufuli imara.
(iv) Vyombo vya chakula (sahani ya mfupa au ya bati, bakuli, kijiko na kikombe – Vifaa hivi vinapatikana kwenye duka la shule kwa bei ya soko aidha vyombo vya plastiki haviruhusiwi).
(v) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko kwa ajili ya matumizi binafsi ya mwanafunzi– Zinapatikana kwenye duka la shule.
(vi) Aje na dawa ya meno, mswaki na mafuta ya kujipaka (mwanafunzi haruhusiwi kutumia vipodozi vya aina yoyote ile pamoja na mapambo).

(vii) Aje na saa ya mkononi kwa ajili ya kutunza muda **(saa zenye marembo pamoja na zile za simu hazikubaliki kabisa!!!).**

(viii) Aje na madaftari makubwa (counter books) nane (8) pamoja na madaftari madogo madogo kumi (10) tu **(utapata kwenye duka la shule)**.

(ix) Aje na mkebe (mathematical set) moja (1)

(x) Aje na non - programmable calculator "kwa wale wanaochukua masomo ya sayansi, jiografia, uchumi na hesabu".

(xi) Iwapo mwanafunzi anasoma masomo ya sayansi aje na "Dissection kit' seti moja tu kwa ajili ya kufanya practical za biology ambapo vifaa hivyo ataondoka navyo pindi amalizapo shule kwani siyo mali ya shule.

(xii) Aje na tochi moja (1) yenye kutumia mawe (battery) au taa zinazotumia mwanga wa jua aina ya D'light S2. Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuja na taa inayotumia umeme, mafuta ya taa au kuja na mishumaa pamoja na kibatari hayaruhusiwi kabisa.

(xiii) Mwanafunzi aje na Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu yake pale anapougua au anapohitaji matibabu.

**Angalizo**: Tochi au taa inayotumia mwanga wa jua itasaidia iwapo umeme utakatika wakati mwanafunzi akiwa darasani au bwenini nyakati za usiku.

## Vifaa vya USAFI:

(a) HGE: Aje na kwanja jipya lililonolewa, jembe moja lenye mpini imara, ndoo kubwa ujazo wa lita 20 pamoja na ufagio aina ya chelewa.

(b) HGK: Aje na kwanja jipya lililonolewa, softbroom, jembe moja lenye mpini imara, pamoja na ufagio aina ya chelewa.

(c)HKL: Aje na kwanja jipya lililonolewa, squeezer, jembe moja lenye mpini imara, pamoja na ufagio aina ya chelewa.

(d) HGL: Aje na kwanja jipya lililonolewa, panga moja tu lililonolewa vizuri, jembe moja tu jipya lenye mpini imara pamoja na ufagio aina ya chelewa.

(e) PCB: Aje na kwanja jipya lililonolewa, hardbroom moja tu, jembe jipya lenye mpini imara, ufagio aina ya chelewa na ndoo kubwa ujazo wa lita 20.

(f) CBG: Aje na kwanja jipya lililonolewa, Reki, ndoo kubwa ujazo wa lita 20 pamoja na ufagio mmoja tu mpya aina ya chelewa.

Aidha mzazi /mlezi unaweza kumpatia mwanao kiasi kidogo cha fedha kulingana na mahitaji yake madogo madogo ya lazima. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na fedha nyingi na iwapo kuna ulazima wa kumtumia mwanao fedha kwa matumizi yake binafsi tumia njia ya posta kwa EMS kupitia anwani hii:-

Jina la mtoto (anayetumiwa fedha)
Nangwa sekondari, (Jina la shule)
S.L.P 34,

**Katesh,(fika posta iliyo karibu nawe kupata maelekezo ya kutuma fedha).**

Angalizo:-**Mzazi/Mlezi hurusiwi kabisa kutumia Akaunti ya shule, mabasi au njia ya simu (M-Pesa, Tigo pesa, Airtel money, Halopesa kutuma fedha kwa ajili ya matumizi binafsi ya mwanao.**

**3. MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA KURIPOTI.**

- **Wakati wa usajili mwanafunzi anatakiwa kuwa na nyaraka zifuatazo kwa ajili ya uthibitisho:-**

- Sare ya shule ya darasani (full school uniform)
- Barua yake ya maagizo (joining instruction)
- Vyeti vyake halisi (originals) na vivuli (photocopies) ya vyeti vya taaluma kidato cha nne (IV) pamoja na leaving certificate (cheti cha kuhitimu kidato cha nne (IV)
- Cheti cha kuzaliwa halisi na kivuli chake
- Barua ya mzazi/mlezi ya kukubali nafasi hii ikiwa imejazwa kikamilifu. (**Kiambatisho B).**
- "Medical Examination form" ambayo imejazwa vizuri na mganga wa hospitali ya serikali na siyo hospitali binafsi (Kiambatisho C).
- Picha nne (4) za wazazi na ndugu wenye mahusiano ya karibu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.
- Maelezo binafsi ya mzazi/mlezi kuhusu historia ya mwanafunzi pamoja na mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai utakaojazwa na mwanafunzi pamoja na mzazi/mlezi

***ONYO NA MAZINGATIO!!***

- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani.
- Mwanafunzi haruhusiwi kwenda bwenini kabla ya kukamilisha usajili wake
- Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi au kitu chochote kinachohusiana na simu, iwapo atakamatwa na simu au kifaa chochote cha Simu atanyang'anywa na **KUFUKUZWA** shule **(hatarejeshewa simu au vifaa hivyo).**
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na chakula cha aina yoyote ile shuleni.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na pasi, heater, kibatari, karabai, mishumaa, radio, camera, television, jiko lolote la kupikia na sufuria, chupa za chai. **NI MARUFUKU.**
- Mwanafunzi hatakiwi kuchelewa shule kwa tarehe iliyopangwa na iwapo atachelewa kwa muda wa siku saba (7) baada ya tarehe ya mwisho ya kuripoti bila taarifa ya maandishi atakuwa amepoteza nafasi yake.
- Mwanafunzi haruhusiwi kufuga kucha, kuweka kucha za bandia, kope za bandia, kupaka rangi kwenye kucha,lipstick, kupaka wanja, kuweka dawa kwenye nywele, kutumia vipodozi na kutumia manukato, haruhusiwi kufuga nywele hivyo atatakiwa kunyoa nywele zake na ziwe fupi muda. Haruhusiwi kunyoa kipara wala panki.

- Atatakiwa kuheshimu viongozi, wazazi/walezi, wafanyakazi wote na jamii kwa ujumla.
- Atatakiwa kuhudhuria vizuri shughuli zote za ndani na nje ya darasa au ya shule.
- Atatakiwa kutekeleza kwa makini na kwa uaminifu na uadilifu mkubwa shughuli zote za shule za jioni kama ilivyo kwenye ratiba.
- Atatakiwa kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine atakazopangiwa
- Atatakiwa kukimbia mara aitwapo na mtu anayemzidi umri.
- Atatakiwa kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo yote juu ya kuwepo ndani au nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wake katika shule hii
- Atatakiwa kutunza usafi wa **mwili** na **mavazi** pamoja na **mazingira** yote ya shule.
- Atatakiwa kuvaa sare ya shule iliyo ndefu na safi wakati wote anapokuwa ndani au nje ya mipaka ya shule.
- Atatakiwa kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ambapo ratiba ya shule huanza saa **11:00 alfajiri kwa mchakamchaka na kuishia saa 4:30 usiku baada ya ukaguzi (Bed checking) ambapo taa zote za ndani ya mabweni na madarasani huzimwa na wanafunzi kulala.**
- Mwanafunzi anatakiwa:- kusoma, kuelewa , kuzishika na kuzifuata sheria za shule ambazo atafafanuliwa kwa kina mara tu afikapo shuleni kwani maonyo na mazingatio hayo yaliyotajwa ni baadhi tu kati ya sheria na taratibu zilizopo na zinazotakiwa kufuatwa.

Ni vyema mwanafunzi kusindikizwa na mzazi/mlezi wake ili mzazi au mlezi huyo afahamu mazingira ya shule na mahali shule ilipo na vilevile kufahamiana na watumishi wa shule na kuwa na uhakika ya kuwa mtoto wake amefika salama mahali panapostahili.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**MAMBO /MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
(vi) Kusuka nywele, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
(vii) Kufuga ndevu
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
(ix) Uvutaji wa sigara.
(x) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba
(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xv) Kumili, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
(xvi) Kudharau bendera ya Taifa
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xviii) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

Aidha shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na**. 25 ya mwaka 1978** na marekebisho yake **Na. 10 ya mwaka 1995**, vile vile shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

Mwisho Kwa niaba ya jumuiya ya Nangwa Sekondari, napenda kukukaribisha sana hapa shuleni na kukutakia safari njema na mafanikio mema katika masomo yako ya kidato cha V na VI.

Kauli mbiu ya shule hii Ni:-

**"Elimu ni ufunguo wa maisha bora ya baadaye" (Education is the key for a better future).**

AHSANTE.

.................

MANYA.A.S

(MKUU WA SHULE)

**Nakala:**

1. Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi,
S.L.P 9121,
**Dar – Es – Salaam.**

2. Katibu Mkuu,
OR – TAMISEMI
S.L.P 1923,
**Dodoma.**

3. Mkaguzi Mkuu wa shule,
Kanda ya Kaskazini Magharibi,
S.L.P 807,
**Arusha**

4. Katibu Tawala Mkoa,
S.L.P 310,
**Babati**

5. Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Hanang',
S.L.P 2,
**Hanang' –Manyara**

6. Mwenyekiti wa Bodi ya Shule

7. Jalada la Shule – **Kumbukumbu.**

**<u>KIAMBATISHO A</u>:**


(i) Sample ya kitambaa – TAZAMA KITAMBAA KILICHOAMBATISHWA HAPO CHINI:-

(a) Sare ya darasa (rangi ya blue bahari ambayo ni sawa na kifuniko cha chupa ya maji ya Kilimanjaro).


(b) Sare ya kazi (rangi nyeusi)

(ii) Mshono wa sketi utakuwa kama hapo chini:- (Sketi ya darasani na sketi ya kazi)

(a) MBELE




(b) NYUMA




**KARIBU SANA NANGWA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA!!!!!!!!.**

**AHSANTE.**

**………………**

**A.S. MANYA**

**(Mkuu wa shule)**

# KIAMBATISHO B.
# SHULE YA SEKONDARI NANGWA

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE KIDATO CHA TANO PAMOJA NA MASHARTI YAKE MWAKA …………

A: MWANAFUNZI

Mimi……………………………………………. nimesoma kwa makini maagizo ya kujiunga na shule ya Sekondari Nangwa, pia nimesoma na kuelewa vema sheria za shule. Kwa heshima na taadhima na unyenyekevu mkubwa ninakubali/sikubali nafasi hiyo pamoja na masharti na sheria za shule kwa sababu zifuatazo:- (**Iwapo unakubali nafasi hii toa sababu vivyo hivyo kama unakataa nafasi hii toa sababu).**

**……………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………**

Tarehe:……………………………………… Saini:…………………

**B:MZAZI/MLEZI**.

Mimi…………………………………………… mzazi/mlezi wa ……………………………. ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Nangwa, nimesoma kwa makini maagizo ya shule na sheria zake na kuzielewa vema. Ninakubali/ninakataa nafasi hiyo,ninaahidi/siahidi kumtimizia mtoto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule kwa muda uliopangwa.

Aidha naahidi/siahidi kushirikiana daima na uongozi wa shule katika **kumkuza, kumlea** na **kumuendeleza** mtoto huyu **kiroho**, **kimwili** na **kiakili** kwa manufaa yake binafsi, wazazi, jamii na Taifa kwa ujumla.

Kama unakataa eleza sababu:-

…………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………

Ahsante.

Jina la mzazi/mlezi:………………………………………………………
Anwani:……………………………………………………………………..
Namba ya simu ya mkononi:………………………………………………..
Tarehe:……………………………. Saini:……………………………….

**Ndugu (3) watatu tu watakaoruhusiwa kumtembelea mtoto/mwanafunzi.**

Mimi mzazi/mlezi nathibitisha kuwa waliojiandikisha hapo chini ni ndugu zangu kabisa ambao wanaweza kuruhusiwa kumtembelea mtoto wangu na siyo vinginevyo.

Jina la mzazi/ mlezi:………………………….. saini:………………..

| S/N | MAJINA MATATU | UHUSIANO WAKE NA MTOTO. | ANWANI | SIMU YA MKONONI | SAHIHI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | |
| 2 | | | | | |
| 3 | | | | | |

***Kata lisilohusika.***

**N.B Sehemu 'B' ijazwe na kusainiwa na mzazi/mlezi na si vinginevyo.**

**………………………**
**A. S. MANYA**
**(Mkuu wa shule)**

# KIAMBATISHO C
# NANGWA SECONDARY SCHOOL
# REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

NANGWA SECONDARY SCHOOL,
P.O.Box 34,
KATESH-HANANG'
**MANYARA**
**DATE:…………………………**

Ref. No. NSS/ME/VOL.I/ FV/2024

TO THE MEDICAL OFFICER,
…………………………………..
…………………………………..
………………………………… (**GOVERNMENT HOSPITAL).**
**STUDENT'S NAME:………………………………… AGE:………. YEAR:……..........**
***Please examine the above named student and arrange for any necessary treatment for student if need be.***

**…………………..**
**A.*MANYA.***
*(THE HEADMISTRESS)*

**MEDICAL CERTIFICATE.**
(To be completed by the medical officer)
I have examined the above named with regard to:

**REMARKS**

**SKIN…………………………………………………………………**
**EYES…………………………………………………………………**
**EARS ……………………………………………………………….. **
**TEETH………………………………………………………………**
**B/S TEST (CHRONIC)…………………………………………………**
**PRESSURE………………………………………………………….**
**ABDOMEN………………………………………………………….**
**CHEST……………………………………………………………….**
**STOMACH…………………………………………………………..**
**URINE……………………………………………………………….. **
**HB.HAEMOGLOBIN…………………………………………………**
**TB TEST………………………………………………………………**
**VDRL…………………………………………………………………**
**HIV TEST……………………………………………………………**
**UPT TEST……………………………………………………………**
**STOOL………………………………………………………………..**
**ULCERS………………………………………………………………**
**DIABETIC ……………………………………………………………**
**ASTHMATIC ………………………………………………………..**
**DISABILITIES (If any)…………………………………………………**
**ALLERGIES (If any)……………………………………………….....**
**ADDITIONAL INFORMATION**
**Eg. Any physical effects or impartment infections, chronic of family disease etc.**

1. **The student is in good health free from infection diseases and is fit to proceed with studies.**
2. **The student will be attending treatment for……………………………………**
   **SIGNATURE ………………………………………………………………..**
   **DESIGNATION…………………………………………………………….**
   **STATION ……………………………………………………………………**

   ***NOTE:*** MEDICAL OFFICER
   ***At the time of Examination, please treat the individual for any ailment you note.***

# KIAMBATISHO D

## ORODHA YA MAJINA YA VITABU VINAVYOTAKIWA KUSOMWA NA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO NA SITA MASOMO YA SAYANSI JAMII NA SAYANSI

**GENERAL STUDIES**

1. **G.S for advanced level certificate**
   *By Richard R.F Mbalase*
2. **The first decade of Mult – Party politics in Tanzania**
   *By Pius Msekwa.*
3. **Corruption and drug Trafficking in Tanzania**
   *By Tanzania chamber of commerce industry and Agriculture (TCCIA)*
4. **Life Skills Manual**
   *By Peace Corps*

**GEOGRAPHY I**

1. **Physical Geography**
   *By R.Bunnet*
2. **Physical Geography**
   *By Msabila*
3. **Physical Geography**
   *By John M. Prichard*
4. **Practical Geography**
   *By John M. Prichard*
5. **Practical Geography**
   *By Zisti Kamili*
6. **Topographical Map, statistics and survey**
   *By Brich, L (1961)*

**GEOGRAPHY 2**

1. **Human & Economic Geography**
   *By D.T. Msabila; Nyambari Nyangwine Publishers.*
2. **Human & Economic Geography**
   *By Gillian; Morgan*
3. **Human Geography, landscape of Human activities**
   *By Fell mann Getis, Getis*

3. **Synoptic literature Wamanda**

**ECONOMICS 1&2**

1. **Economics Advanced Level Paper 1 and 2**
   *By – M.C. Ambilikile; Nyambari Publishers.*

2. **Modern Economics**
   *By – Robert Mudida; Focus Publishers ltd*

3. **Principle of economic**
   *By – Salvatore D. Diulo*

**BASIC AND APPLIED MATHEMATICS (BAM)**

1. **Basic Applied Mathematics**
   *By Respicious Kiiza*
2. **Basic Applied Mathematics Review; questions and solutions (BAM)**
   *By Emmanuel Kimbe.*

**SCIENCE SUBJECTS:-**

**(I) PHYSICS**

- (i) Nelcon and Parker (A level physics)
- (ii) Advanced Physics (Tom Duncan)
- (iii) Chand's (XI&XII)

**(II) CHEMISTRY**

- (a) Conceptual chemistry by Chandy
- (b) Organic chemistry by Chandy
- (c) Physical chemistry by Zumdahil
- (d) TIE books – Organic chemistry
  - Inorganic chemistry
  - Physical chemistry

**(III) BIOLOGY.**

- a. Chandy Biology for class XI and XII
- b. Understanding Biology
- c. Biology0 foy form 5 and 6 by Ernest Kira.

……………………………
A.S MANYA.
(Head of School)